# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA FEDHA, BIASHARA NA KILIMO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,**
Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu, ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa ndani ya Baraza lako tukufu, tukitekeleza majukumu yetu ya msingi ya kuwatumikia wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**
Nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa uwasilishaji wake wa makini wa hotuba ya bajeti kwa wakati unaostahiki sambamba na kuipatia Kamati ufafanuzi kila ilipohitajika. Ni dhahiri kuwa maelezo ya kina yaliyomo kwenye taarifa hiyo yameisaidia sana Kamati kuelewa na kujiridhisha juu ya shughuli za Wizara na fedha za Mapato na Matumizi zilizotengwa kwa mwaka 202/2021.

**Mheshimiwa Spika,**
Tangu mwaka jana 2019 na mwaka huu 2020 misimu ya mvua imebadilika na kupelekea mazingira mazuri kwa wakulima wa mazao mbalimbali nchini na ni hali ambayo haijatokea siku nyingi mvua za vuli kuendelea kunyesha mpaka mwezi wa Februari mwaka uliofuata na kuunganika na masika. Kadhalika, Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua kubwa za kazi za maendeleo ilizozifanya katika kipindi kilichopita ikiwemo ununuzi wa mtambo wa chakula cha kuku jambo ambalo litawaondolea usumbufu wafugaji wetu na kujiamini katika shughuli zao za ufugaji.

Aidha, pembejeo za kilimo zimepatikana kwa wakati mwaka huu jambo ambalo limewapa faraja wakulima wetu nchini. Kamati inasisitiza ugawaji wa pembejeo hizo

ufanyike kwa kuzingatia vigezo madhubuti ili kuzigawa kwa wakulima na kupelekea kuongezeka ufanisi wa kazi zao pamoja na kukuza pato la Taifa. Kamati pia inaunga mkono na kuzipongeza juhudi za wakulima wa matunda na mboga nchini kwa kasi ya uzalishaji waliyonayo jambo ambalo limepelekea upatikanaji wa matunda kwa karibu misimu yote ya mwaka na kuimarisha afya za wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**
Bila ya kupoteza muda, naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambao walitoa mchango na ushauri mkubwa katika utekelezaji wa kazi za Kamati kwa Wizara hii, Wajumbe wenyewe ni:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Dkt. Mwinyihaji Makame | Mwenyekiti; |
| 2. | Mheshimiwa Hamida Abdalla Issa | Makamo Mwenyekiti; |
| 3. | Mheshimiwa Ahmada Yahya Abdulwakil | Mjumbe; |
| 4. | Mheshimiwa Moh'd Mgaza Jecha | Mjumbe; |
| 5. | Mheshimiwa Mussa Ali Mussa | Mjumbe; |
| 6. | Mheshimiwa Nadir Abdullatif Yussuf | Mjumbe; na |
| 7. | Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir | Mjumbe. |

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yetu pia inashirikiana ipasavyo na makatibu wawili (2) ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia kutekeleza majukumu yetu, kwa heshima naomba niwatambue makatibu hao ni:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndugu Asma Ali Kassim | Katibu |
| 2. | Ndugu Said Khamis Ramadhan | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yetu ilipitia, kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Fungu L01 la Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na kufanya marekebisho madogo madogo kwa ajili ya kuijenga zaidi. Kiujumla, Makadirio ya Mapato ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2020/2021 ni sawa sawa na makadirio ya mapato kwa mwaka 2019/2020 ambayo ni jumla ya shilingi bilioni 10,468,264,000.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa upande wa matumizi, Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 129,862,460,000 kwa mwaka 2020/2021 ambalo ni ongezeko la shilingi bilioni 41,689,160,000 kutokana na makadirio ya mwaka 2019/2020. Makadirio hayo yanadhihirisha wazi kuwa bado sekta ya kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu. Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuendelea kuipa kipaumbele sekta ya Kilimo na kuhakikisha uwepo wa chakula kwa muda wote nchini na kumpiga vita adui njaa.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, mapato ya rasilimali ya mchanga, Mawe na Kokoto (Vifungu namba 1422023) yanakadiriwa kupungua kutoka shilingi bilioni 7,692,524,000 hadi shilingi bilioni 6,700,764,000. Hali hiyo inatokana na mwelekeo wa Serikali kujiandaa na mpango wa kuyaruhusu makampuni makubwa nchini kuagiza mchanga kutoka nje ya Zanzibar ili kuwapa fursa wazawa kunufaika na rasilimali hiyo kikamilifu. Tunaipongeza Serikali kwa hatua ya kuwanusu Wazanzibari wengi wanaotegemea maisha yao kwa kufanya shughuli mbalimbali zinazotumia rasilimali ya mchanga wakiwemo mafundi ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilishangazwa na kushuka kwa mapato ya kifungu kidogo (L0109) ya Taasisi ya Utafiti wa kilimo Kizimbani kutoka shilingi milioni 104,160,000 mwaka 2019/2020 hadi shilingi milioni 95,000,000 kwa mwaka 2020/2021 ikiwa ni nakisi ya jumla ya shilingi milioni 9,160,000. Nakisi hiyo ni kubwa tukizingatia kwamba Taasisi yenyewe ni changa na inahitaji rasilimali nyingi ili iweze kusimama na kuendesha majukumu yake ipasavyo. Hata hivyo, tunaipongeza Serikali kwa kuleta hapa Barazani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Utafiti wa Kilimo (tayari umeshatiwa saini na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi) ambao kwa kiasi kikubwa utaisaidia Taasisi hii kukusanya mapato na kuandika maandiko tofauti kwa Washirika wa Maendeleo yatakayoitangaza na kuiongezea mapato Taasisi hii. Kamati yetu inamatumaini makubwa na Taasisi hii kwamba iwapo itajipanga vizuri, itaweza kufanya mageuzi makubwa katika maendeleo ya kilimo na misitu katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa upande wa Makadirio ya Mapato ya Uvuvi wa Bahari Kuu kifungu (1422067) yameongezeka kutoka shilingi bilioni 1,526,080,000 mwaka 2019/2020 hadi shilingi bilioni 2,500,000,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati yetu imeshangazwa na ongezeko hili la asilimia 61 zinazotegemewa kukusanywa kutokana na kuzorota kwa ukatishaji wa leseni za uvuvi wa bahari kuu wakati dunia ikiwa katika vita dhidi ya ugonjwa wa corona na mporomoko wa uchumi.

**Mheshimiwa Spika,**
Ni matumaini ya wananchi wa kawaida kuwa mara tu baada ya Serikali kununua meli yake ya uvuvi wataondokana na shida ya kitoweo. Ni jambo lisiloweza kuyumkinika kuona hadi wakati huu ambapo meli hiyo tayari imepatikana (Sehewa 2) bado wananchi hawajaona matunda na faida moja kwa moja inayotokana na uwepo wa meli hiyo. Hivyo, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaishauri Wizara kuwauzia wananchi wa kawaida samaki wanaowavua ili nao wafaidi matunda ya nchi yao kama ilivyokuwa hapo awali ambapo Serikali ilikuwa ikiuza vitoweo kwenye vibanda maalum vilivyojengwa nchini kote.

**Mheshimiwa Spika,**
Kuhusu mpango wa uzalishaji samaki nchini unaosimamiwa na Mradi wa uzalishaji na ugawaji wa vifaranga vya samaki ambao kwa hatua ya awali tayari umeshaanza uzalishaji wa rasilimali hiyo na kuviuza kwa wananchi wetu. Kamati yetu haikufurahishwa na taarifa kuwa baadhi ya maeneo na vikundi vilivyopatiwa vifaranga hivyo wameshindwa kuvilea na kuvikuza na hatimaye vifaranga hivyo vimekufa bila ya kufahamika kwamba vifaranga hivyo vilizalishwa chini ya kiwango au ni uchache wa matayarisho na elimu kwa wakulima wetu waliokabidhiwa. Ipo haja kwa Wizara kujipanga vizuri kwa miradi kama hii nyeti na inayogharimu fedha nyingi ikiwa ni pamoja na kuwapatia elimu wananchi wetu kabla ya kukabidhiwa vifaranga hivyo.

**Mheshimiwa Spika,**
Kuna kazi kubwa na nzuri imefanywa na Kamati ya Kitaifa ya Ugunduzi wa Mashamba ya Serikali ya Mikarafuu Kisiwani Pemba ambayo ilisaidiwa sana katika utekelezaji wa majukumu yake na Kamati ya ndogo ya Ufichuaji Mashamba iliyoundwa na wanajamii waliyokuwa wakiyatambua maeneo yaliyopo mashamba husika na kufanikiwa kufichua mashamba zaidi ya 300 yaliyokuwa katika mikono ya watu tofauti wakiyamiliki kinyume na utaratibu. Kamati yetu ilielezwa kwamba baada ya kazi hiyo kumalizika, Baadhi ya wajumbe wa Kamati ndogo ya wanajamii waliielezea Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia Ofisa Mdhamini Pemba kuhusu madai yao ya kufidiwa chochote kutokana na kazi kubwa waliyoifanya hasa ukizingatia walitumia fedha zao mfukoni kuwalipa baadhi ya watu waliowaonesha mashamba hayo ambapo hadi Kamati inakutana na Kamati hiyo, walikuwa hawakamilishiwa madai yao.

**Mheshimiwa Spika,**
Ni busara kwa Wizara ya kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kukipokea kilio cha wajumbe wachache wa kamati hiyo na kukifanyia kazi ipasavyo ili kuondosha malalamiko yasiyo ya lazima kwani tunafahamu kuwa Serikali yetu ni sikivu sana katika kusikiliza na kuvifanyia kazi vilio vya wananchi wake. Sambamba na hilo, Kamati yetu pia inaisisitiza Wizara kwamba changamoto zilizojitokeza katika ufichuaji wa mashamba pamoja na mchakato mzima wa ukodishaji wake ikiwemo kutojulikana kwa mipaka ya mashamba, zifanyiwe kazi kwa haraka ili msimu ujao zisijitokeze tena na mashamba

hayo yakodishwe na fedha zitakazopatikana ziingizwe katika Mfuko Mkuu wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, namtakia mafanikio mema Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika bajeti yake ya mwaka 2020/2021 na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waichangie, waihoji, waikosoe na hatimae waipitishe bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo, naunga mkono kwa asilimia Mia Moja Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya mwaka wa fedha 2020/2021 na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

………………………,
Mhe. Hamida Abdalla Issa,
Kny: Mwenyekiti,
Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**